**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0717199833**

**Makamu Mkuu wa Shule0710191115**

**Matron/Patron0658271871/0754507660**

**Shule ya Sekondari Itipingi**

**S.L.P 600**

**Tarehe26/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ITIPINGI HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya PCB(Physics,Chemistry na Biology)

Shule ya Sekondari Itipingi ipo umbali wa Kilometa 12 Kusini Mashariki mwa Mji wa Makambako, Usafiri wa basi kutoka mjini Makambako unapatikana katika kituo cha mabasi Nauli ni Shilingi 3000/=kwa pikipiki na bajaji nauli ni Tsh 10000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01 July 2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30 June 2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 16 July 2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

**KWA WAVULANA**

Sare ya shule hii ni

i. -suruali 2, moja rangi ya kaki na ya pili rangi ya damu ya mzee

ii -mashati 2 meupe mikono mifupi

iii -tishirt 2 rangi ya blue, suruali 2 nyeusi (shamba dress)

iv -sweta 2 kijani jeshi

v -track suit 1 rangi ya blue bahari na track suit nyingine kwaajili ya kulalia na kujikinga na baridi rangi dark blue

vi -viatu vyeusi jozi 2 vya kufunga kamba

vii -soksi pair 2 nyeusi

viii. mkanda mweusi wa kubvalia suluari

**KWA WASICHANA**

i. -sketi 2 zenye malinda 7 kila moja, moja rangi ya kijani jeshi naya pili rangi ya damu ya mzee,sketi ifike kwenye magoti

ii. -suruali 2, moja kijani jeshi na ya pili damu yam zee(isiyobana)

iii. - mashati 2 meupe mikono mifupi

iv. -gauni 2 ndefu rangi ya pink zenye kola nyeupe ,mshono wa solo (shamba dress)

v. -sweta 2 rangi ya kijani jeshi

vi. -track suit 1 rangi ya blue bahari na track suit nyingine kwaajili ya kulalia na kujikinga na baridi rangi dark blue

vii. Soksi nyeupe pair 2 na viatu vyeusi pair 2 vya kufunga kamba

viii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 countre book kuanzia Quire 3
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
*iii.* Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa)*
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro kwa wanafunzi liwe la ft mbili na nusu

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
viii. Nguo za ndani ziwe za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
xii. Tochi ya solar kwa matumizi yake ya usiku(ingawa umeme upo)
xiii. Lab coat( kwa ajili ya masomo ya vitendo yanayofanyika maabara)
xiv. Koti jeusi lisilovuka magoti kwa ajili ya kujikinga na baridi

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**Michango mbalimbali na italipwa kwenye account ifuatayo:-**
**NMB acount no 60301100005 Jina ITIPINGI SECONDARY SCHOOL**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ......................................**

**Jina la Mkuu wa Shule .....................................**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule .................................**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule0756 866 468/0717 199 833**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0710 191 115**
- **Mwandamizi Taaluma 0678 022 288**
- **Mwandamizi Malezi 0769 980 956**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAISI TAWALA ZAMIKOA NA SERIKALI ZA MITAA MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A: MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI………………………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………………….

3.Mahali alipozaliwa ……………………………………………………..

(Wilaya) …………………….. (Mkoa) ……………………………………………..

4.Dini………………………………………………………………………………………

Dhehebu ……………………………………………………………………………..

B: MZAZI/MLEZI ANAYEKUTUNZA

JINA………………………………………………………………………………………

KAZI………………………………………………………………………………………

ANUANI…………………………………………………………………………………

ANAPOISHI Wilaya …………………………………………………….

Kijiji ……………………………………

Kata …………………………………..

C: JINA LA ANAYEKULIPIA ADA/KARO YA SHULE

JINA……………………………………………………………………………………………

UHUSIANO.................................ANUANI …………………………………………….

SIMU ………………………………………………………………………………………..

D: AFISA MTENDAJI/KATIBU KATA

JINA……………………………………………………………………………………… ……… KATA…........................................................Wilaya …………….Mkoa…......................... Nathibitisha kuwa mwanafunzi ………………………………………………………ni mkazi wa kata hii na ni raia wa Tanzania. SIMU… ......................................................................................... Sahihi ………………………………Muhuri ………………………tarehe ………………….

JINA LAMWENYEKITI WA MTAA/KIJIJI

JINA…..............................................................MTAA/KIJIJI ……………………………………….KATA …………………………WILAYA…………………… MKOA ……………….

Nathibitisha kuwa mwanafunzi.......................................................................... ni

mkazi wa mtaa/kijiji hiki na ni raia wa Tanzania. SIMU ……………………………………………………………………………

FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

I. MWANAFUNZI

1. Mimi…......................................................................................kidato cha ……………………....................

2. Nakubali kujiunga na shule hii ya Sekondari ITIPINGI nikiwa mwanafunzi wa Bweni

3. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote, sharia na taratibu zote za shule. Nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya Sekondari ITIPINGI. 4. Kwahiyo naahidi kwamba:- a) Nitazitii sharia zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu. b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vita kuwa kinyume na uongozi wa chama tawala na Serikali ya Jamuhuri ya Muunganoawa Tanzania. c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na mazingira, samani (furniture), vitabu n.k d) Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu. e) Nitashiriki katika shughuli zingine za nje mbali na masomo ya darasani.

Sahihi ya mwanafunzi……………… tarehe ………………………………

II. JINA LA MZAZI/MLEZI Mimi ……………………………………………………………………………….. ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………………… kidato cha …………… mwaka …………. tarehe …..……………… akiwa mwanafunzi wa Bweni/Hostel. Kwahiyo naahidi:- a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule walimu na wafanyakazi wengine katika kumuelimisha na kumkemea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sharia na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hao juu. b) Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulu kwa muda wote awapo shuleni.

Anuani yangu ya kudumu ni ................................................ Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………. tarehe …………………

KUWATEMBELEA WANAFUNZI/SIKU YA WAGENI Wazazi / walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa mwezi ambao ni kila Jumapili yamwisho wa mwezi kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 10:30 jioni. Mwalimu wa zamu atakuwepo shuleni kwa muda huo kupokea wageni; hairusiwi kumletea mwanafunzi chakula

ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

**A: CHEMISTRY**

1. Advanced Chemistry Review by William W. Davis (Mzumbe bookshop project, 2004)
2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe bookshop project, 1998)
3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II. (Tanzania institute of education, 1995)
4. Organic Chemistry Volume I. The Fundamental Principles by I.L Finar (Longman Ltd 1990)

**B: BIOLOGY**

Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia

1. New understanding Biology b Suzan Toole
2. Advanced Biology by Michael Kent
3. Biological science third by D.J. Taylor, N.P. O Green and G.W.stout.
4. Advanced Biology Principle and application by C.J Clegg and DG Mc Kean.
5. New understanding Biology for advanced level by Glenn and Susan Toole.
6. Plant and Animal Biology volume 1 & 2 by AE vines and N Rees.
7. Biology for class XI & XII by Dr. P.S Verma and Dr. B.P Pandey.

**C. PHYSICS**

1. Scientific calculator
2. Advanced Level Physics (4th Edition) (1993) by Muncaster
3. Principle of Physics for Class XII (2007) By Metha, V.K & Methar R.
4. Advanced Physics (5th Edition). (2000) by Duncan, T.

**D. BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic applied mathematics by Kiza and septine I sillem.
2. Basic applied mathematics by TIE
3. Core course Mathematics By Bostoch and chandler

**E. GENERAL STUDIES**

1. General studies for A – level certificate form V.
2. Contemporary approach for A level general studies notes for form V and VI.
3. General Studies Supplementary Book for A level and Colleges.
4. Advanced level general studies notes form V & VI by Nyambari Nyangwine 200

FOMU NA.3. MEDICAL EXAMINATIONS. (To be completed by medical officer only)

1. Pupil's name
……………………………………………………………………………………………….

2.
Age…………………………………………………………………………………………………
………..

3. Blood count (white and red)………………………………………………………………………….

4. Stool examination
………………………………………………………………………………………..

5. Syphilis or/and other venereal diseases test ……………………………………………………

6. T.B test
……………………………………………………………………………………………………
………..

7. Eye test
……………………………………………………………………………………………………
………..

8. Ears
……………………………………………………………………………………………………
……………..

9. Abdomen
……………………………………………………………………………………………………
……

10. Spleen
……………………………………………………………………………………………………
………..

11. Urine for plamo test
……………………………………………………………………………………….

ADDITIONAL INFORMATION If any e.g physical defeats, impairment, infections, pregnancy, chronic or family diseases etc
……………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………

III. I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

STATION ..........................................................................................................................


SIGNATURE……………………….........................................................................................

DATE……………...…...…..DESIGNATION…...........................................................................


OFFICIAL STAMP…………………………..........................................................................



**KITAMBAA CHA RANGI YA DAMU YA MZEE**



**KITAMBAA CHA RANGI YA KIJANI KIJENSHI**



**KITAMBAA CHA RANGI YA KAKI**